



TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA
HALMASHAURI YA WILAYA YA KILWA



Unapojibu tafafhali taja:

Kumb: Na. KDC/L.10/36/88

03/09/2021

TANGAZO LA NAFASI ZA KAZI.

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Kilwa anayo furaha kutangaza nafasi 03 za ajira ya kudumu kwa wataanzania wote wenye sifa stahiki. Nafasi za ajira hizi zinatokana na Kibali cha ajira mbadala kutoka kwa **Katibu Mkuu, Ofisi ya Rais, Menejiment ya Utumishi wa Umma na Utawala bora** kwa barua Kumb. Namba **FA.170/372/01/"A"/65** ya tarehe **02 Agosti, 2021.**

1. MTENDAJI WA KIJIKI III - Nafasi 03

1.1 Kazi Na Majukumu.

- Kuratibu na kusimamia upangaji na utekelezaji wa mipango ya Maendeleo ya Kijiji.
- Kusimamia ulinzi na usalama wa raia na mali zao.
- Kukusanya mapato ya Halmshauri ya Kijiji.
- Kusimamia, kukusanya na kuhifadhi kumbukumbu zote na nyaraka za kijiji.
- Katibu wa mikutano na kamati zote za Halmashauri ya kijiji.
- Kusimamia utungaji wa sheria ndogo za kijiji.
- Afisa masuhuli na Mtendaji Mkuu na Serikali ya kijiji.
- Kupokea na kusikiliza na kutatua malalamiko na migogoro ya wananchi na
- Kazi nyingine atazopangiwa na mwajiri.

1.2 Sifa Za Mwombaji

- Awe amehitimu elimu ya kidato cha nne au sifa pia awe amehitimu mafunzo ya Astashahada/cheti katika moja ya fani, zifuatazo:- **Utawala, Sheria, Elimu ya Jamii, Usimamizi wa fedha, Maendeleo ya Jamii na Sayansi ya Sanaa**

kutoka katika chuo Cha Serikali za Mifaa Homolo
Dodoma au Chuo chochote kinachotambuliwa na Serikali.

2.0. MASHARTI YA JUMLA

- i) Waombaji wote wawe ni Raia wa Tanzania.
- ii) Waombaji wote wawe na umri kati ya miaka 18 - 45
- iii) Waombaji wote waambatanishe cheti cha kuzaliwa.
- iv) Waombaji waambatanishe maelezo binafsi (CV) yenye anuani na namba za simu za kuaminika na majina mawili ya wadhamini.
- v) Maombi yaambatishwe na picha moja (Passport size ya hivi karibuni na iandikwe jina kwa nyuma).
- vi) Maombi yaambatanishwe na nakala za vyeti vya taaluma/Shule na vyeti vya kuhitimu mafunzo ya vyuo.
- vii) Maombi yote yatumwe kwa njia ya posta kwa kutumia anuani ifuatayo;-

**Mkurugenzi Mtendaji,
Halamshauri ya Wilaya,
S.L.P. 160,
KILWA.**

Mwisho wa kupokea barua za maombi tarehe **16/09/2021 saa 9: 30**
Alasili

NB: Maombi ambayo yatawasilishwa kwa njia ya mkono na kutozingatia sifa tajwa hapo juu hayata shughulikiwa.

Imetolewa na



JUMA J. HAMADI

**KAIMU MKURUGENZI MTENDAJI
HALMASHAURI YA WILAYA KILWA**

**MKURUGENZI MTENDAJI
HALMASHAURI YA WILAYA
KILWA.**

Ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji (W), S.L.P 160, Kilwa--Lindi, Simu: Namba +255 232013065, Fax Namba: +255 232013065, tovuti: www.kilwadc.go.tz, Barua Pepe: ded@kilwadc.go.tz